



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Unapojibu tafadhali taja:-  
Kumb. Na: WDC/A.10/11/53

27 Mei, 2022.

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Kwa mujibu wa Kibali cha Ajira Mpya kilichotolewa na Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging`ombe chenye Kumb. Na. FA.97/228/01/09 cha tarehe 13 Mei, 2022. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging`ombe anawatangazia watanzania wenye sifa na ujuzi stahiki kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo.

### KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III – TGS B (NAFASI 3)

#### Sifa za Muombaji.

Awe amehitimu kidato cha IV aliyehudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za **Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.**

#### Kazi na Majukumu.

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Wakuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

**MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani Mshahara wa **TGS B**

**MASHARTI YA JUMLA.**

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 – 45.
- ii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V.**) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- iii. Maombi yote yaambatane na Cheti cha Kuzaliwa, vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- iv. **Testimonials, "provisional results", "statement of results", hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita HAVITAKUBALIWA.**
- v. Waombaji waambatishe picha moja ya "Passport size" ya hivi karibuni.
- vi. Waombaji waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Uraia au namba ya Kitambulisho hicho kutoka mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- vii. Waombaji ambao walisoma nje ya nchi vyeti vyao vya Taaluma vifanyiwe ulinganishi na TCU na NECTA na majibu ya ulinganisho yaambatanishwe kwenye barua ya maombi ya kazi.

**Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 10 Juni, 2022.**

**Maombi yote yatumwe kwa:-**

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya Wanging'ombe,  
S.L.P. 64,

**NJOMBE.**

Imetolewa na:



Maryam A. Muhaji

**MKURUGENZI MTENDAJI (W).**

**WANGING'OMBE.**

**Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya:-  
[www.wangingombedc.go.tz](http://www.wangingombedc.go.tz)**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA WANGING'OMBE